JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA BIHARAMULO

**Kumb.Na.BDC/2/47/VOL. IV /77** **22/09/2025**

# TANGAZO! TANGAZO! TANGAZO!

**WAFANYA BIASHARA WOTE,**
**WILAYA YA BIHARAMULO.**

## YAH: FURSA MBALIMBALI ZA ZABUNI KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA BIHARAMULO

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo anawatangazia Wafanya BIashara wote wa Wilaya ya Biharamulo kuchangamukia fursa zilizopo katika Halmashauri ya Biharamulo

Halmashauri imekua ikitangaza kazi mbalimbali kupitia mfumo wa Manunuzi NeST, ambapo Mfanya Biashara yeyote anayetaka kufanya kazi za Halmashauri yetu lazima awe amejisajili katika mfumo wa Manunuzi NeST. Kazi au Huduma zinazotangazwa ni kama Ifuatavyo:-

1. MAFUNDI WA UJENZI (LOCAL FUNDI)
2. WAUZAJI VIFAA VYA VIWANDANI
3. WAUZAJI VIFAA VYA UMEME
4. WAUZAJI MADINI YA UJENZI (MCHANGA, MAWE, KIFUSI,MAWE n.k)
5. WAFYATUAJI TOFALI ZA SARUJI ( BLOCK)
6. WAUZAJI WA MBAO AINA ZOTE PIA NA MIRUNDA
7. WATANGAZAJI ( MATANGAZO MBALIMBALI YAKIWEMO YA REDIO)
8. WENYE KUMBI NA NYUMBA ZA KULALA WAGENI

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W), S.L.P 70, Biharamulo, Simu:0282225003, Nukushi: 0282225216,
Barua pepe: ded@biharamulodc.go.tz. Tovuti: www.biharamulodc.go.tz.

9. UTENGENEZAJI MAGARI, PIKIPIKI, GUTA NA MITAMBO
10. KUKODISHA MAGARI
11. KUTOA HUDUMA YA CHAKULA
12. WAUZAJI WA MAFUTA YA MAGARI NA MITAMBO

Ili uweze kupata fursa hizo za kazi unatakiwa kuwa umesajiliwa kwenye Mfumo wa Manunuzi NeST. Pia kazi hizo zinatangazwa na watoa huduma ngazi za chini yani Shule za Msingi na Sekondari, Vituo vya kutolea huduma za Afya na Vijiji

Mkurugenzi Mtendaji (W) anawatangazia fursa hizo wenye nia ya kuomba kazi hizo wafike kupata msaada wa kusajiliwa kwenye Mfumo wa NeST katika Ofisi ya Kitengo cha Manunuzi na Ugavi (W) kilichopo makao makuu ya Halmashauri kila siku ya Alhamisi ya Kila juma
Ili uweze kusajiliwa unapaswa uwe na Vitu vifuatavyo:-

1. LESENI YA BIASHARA
2. TIN NAMBA
3. NAMBA YA SIMU UNAYOTUMIA

**Innocent Mbandwa Mukandala**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
BIHARAMULO

**Nakala :** Mbao zote za Matangazo

Mwenyeki wa Wafanya Biashara **(Kufahamisha Wafanya Biashara)**

Wakuu wa Taasisi Ngazi ya Chini ya Halmashauri

**(bandikeni Tangazo kwenye maeneo yenu)**